Translator: Sr Martina Marco, asc

...Kwa Neno Lako...

Hati, M M 2017

Mwaka XX – Namba 3, Januari 2018

Waabuduo Damu ya Kristo

Bwana uje daima

Mhariri

Unakuja usiku, lakini ndani ya mioyo yetu ni usiku daima: kwa hiyo, njoo daima , Bwana.
Unakuja katika ukimya, lakini sisi hatujui cha kusema zaidi: kwa hiyo njoo daima Bwana.
Unakuja katika upweke, lakini kila mmoja wetu, daima yuko peke yake: kwa hiyo njoo daima Bwana.
Njoo Mwana wa Amani, sisi tunapuuza kile kinachokuwa amani; kwa hiyo njoo daima Bwana.
Njoo utuokoe, sisi tunakuwa zaidi watumwa daima: kwa hiyo njoo daima Bwana.
Unakuja kutufariji, sisi tunakuwa zaidi wenye huzuni daima: njoo daima, Bwana.
Unakuja kututafuta, sisi tunapotea zaidi daima: njoo daima, Bwana.
Unakuja wewe unayetupenda, hakuna aliyekatika ushirika na ndugu kama hayuko nawe kwanza, Bwana.
Sisi sote tuko mbali na wala hatujui sisi ni nani, kitu gani tunapenda; Njoo Bwana.
Njoo daima, Bwana.

p. David Maria Turoldo, Mtumishi Maria

Mhutasari

Mhariri Bwana uje daima

Toka Uongozi Mkuu Karibuni!

Toka Ulimwengu ASC Habari kuhusu Mwenye heri Sr. Sarafina Cingue
Mwenye her Sr Serafina
Barua ya Dorothy Day
Hongera kwa siku ya kuzaliwa!
Changamoto za Mkutano Mkuu 2017

Toka JPIC Anachokuomba Bwana

Kalenda ya Uongozi Mkuu
hongera - pongezi
Waliorudi nyumbani kwa Baba

Ndani ya Shirika



Karibuni!

Tanzania ni nchi ya Afrika Mashariki yenye hali ya hewa ya kitropiki. Nchi ilipata uhuru mwaka 1961 na inakua. Waabuduo wa kwanza wa Kiitaliano waliwasili hapa mwaka wa 1969. Masista wa Region ya Tanzania tayari wameanza mchakato wa kuandaa Jubile ya dhahabu: miaka 50 ya uwepo wa ASC katika nchi hii ya kiafrika yenye kukaribisha na wazi.

Wakati wa kukaa kwetu pale tuliweza kwenda kwenye jumuiya zetu zote na tulikutana na masista wenye furaha, tumaini

Kwa furaha tunapenda kuwashirikisha mang'amuzi yetu mazuri ya ziara kwa masista wa Region ya Tanzania miezi miwili baada ya kuanza kwa utumishi wetu. Kwa upande wa Nadia, hii haikuwa mara ya kwanza kutembelea Region hii, kwa upande wangu kila kitu kilikuwa kipya. Madhumuni ya ziara yetu ilikuwa kuendeleza usindikizaji ulioanzishwa na uongozi mkuu uliopita. Tulitumia muda wetu wa kuwa pale kukutana na masista ili kufahamiana nao kwa karibu na kuzifahamu jumuiya wanamoinsi, utume na utajiri wa hali halisi utamaduni wao. Hizi zilikuwa siku nzuri sana na tulipata fursa ya kukutana na walelewa katika malezi ya mwanzo na kuanza kuangalia malezi kwa mtazamo wa novisiati ya kimataifa. Tulitumia muda mwingi kufanya kazi na Ungozi wa Region na kusaidia katika changamoto wanazopaswa kuzikabili na zinazoonyesha kila uhalisia wa Shirika.

Tuliicha Italia, pamoja na hali yake ya baridi kwa sasa asubuhi ya Novemba 25 na tukafika jioni ya siku hiyo kwenye joto la Tanzania. Siku za joto zilitukaribisha, si tu kama hali ya hewa, lakini juu ya yote kwa mapokezi mazuri ya masista.

na daima wanaotaka kufanya vizuri zaidi. Siku ya masista huanza kila siku mapema sana, kwa masifu na adhimisho la Misa takatifu: huduma ya sala inajidhihirisha kati ya masista na kila mahali tuliona umakini mkubwa katika sala za jumuiya.

Liturujia, inaandaliwa vizuri, ni nafasi ya kumsifu Mungu kwa lugha ya Kiswahili kwa zaburi, nyimbo na muziki mzuri unaoambatana na mapigo ya ngoma na ala za muziki. Miongoni mwa zawadi tofauti za Mungu tuliona mara moja, kwamba kuimba, kucheza na kupiga vyombo ni vipaji mahususi siyo tu vya masista wetu, bali ni vya watu wote wa Tanzania. Wakati wa ziara kwenye jumuiya tuliweza kuona kazi za kitume ambazo masista wanaziendeleza: hasa shule za msingi na za sekondari ambapo mamia ya wanafunzi wa kike wanajifunza na pia dispensari, Kijiji cha Matumaini na Kituo cha Msamaria Mwema. Masista wanafanya kazi hospitalini, wanafanya kazi parokiani, wanashona, wanatafuta njia mbalimbali za kusaidia maskini, hasa watoto. Masista wengi wana-

soma ili kujiandaa kwa ajili ya utume. Kazi nyingi na mahitaji ni mengi; ingawa Region inakua kwa idadi, masista wanakosekana ili kutosheleza mahitaji kazi mbalimbali za kitume na hii ni changamoto kubwa.

Kila siku masista wanamwomba kwa Bwana kwa ajili ya miito ya wale waliotayari kutumtumika " jirani yetu mpendwa".

Wakati tukiwa Dodoma semina ya kwanza ya "Mduara ya Upatanisho" ilifanyika ikiongozwa na Pd. Gregorio CPPS na Sr. Florida ASC. Washiriki walishirikisha nasi furaha ya uzoefu huu wa kina wa kusikiliza kama nafasi ya kufahamiana na safari ya uponyaji wa ndani. Furaha ya kushirikishana kwa njia ya kina na kuwa pamoja kuweka maisha ya kila mmoja katikati, ilitoa kwa kila mmoja nguvu na tumaini jipya.

Wiki mbili zilizoshinda na masista nchini Tanzania zilikuwa ni muda kuingia ndani na wa kutafakari; mikutano na michakato ya uchambuzi ulioanzishwa zimeleta kwetu sisi sote imani na tumaini kuwa Region changa zaidi ya Shirika letu inakuwa na inataka kukua katika kuchukuwa jukumu la kujibu vizuri wito wa Mungu.

Sr Wiesława Pryzbyło, asc

Eneo la Bara: Amerika
Region: Brazili

Habari kuhusu Mwenye Heri Sr. Serafina

Elimu juu ya mpendwa wetu na mwenye Heri Sister Serafina Cinque imepata mafanikio katika mwaka 2017. Don Danilo Rodrigues, padre wa jimbo na mwanafunzi wa zamani wa Shule Msista Waabuduo huko Santarem, Para, na ambayo ametunza urafiki, alitaka kama Paroko wa Parokia ya "Maria, mama wa Kanisa", katika mji Belo Horizonte, mji mkuu wa Jimbo la Minas Gerais - katikati ya Brazil, kumtangaza Sr. Serafina, ambapo yeye ana ibada kubwa kwake.

Kwa hiyo, katika mwezi wa Julai 2017 D. Danilo alipendekeza kwa Sr Marilia Menezes kwamba Harakati ijulikanayo kama "Mkutano wa Wanandoa na Kristo" katika Parokia yake, uwe na msimamizi na kiongozi kama sista wetu Mwenye heri. Kiongozi Bibi Fabiola Cabrale na mumewe walimwomba Sr. Marilia maandiko ya kutosha ili kumfahamu mtu huyu, ambayo yalisomwa kwa muda wa mwezi mmoja. Mkutano, ambao ulihusisha wanandoa 50 kwa siku 3, ulifanyika mnamo Novemba na ulifanikiwa. Fabiola alimtumia Sr. Marilia vitu vidogo vidogo vilivyofanywa na wanandoa walioonyeshwa kwenye maonyesho yaliyofunguliwa wakati wa mkutano; juu ya hayo ni uso wa Sr. Serafina na maneno ambayo yamekuwa ni ishara ya Mkutano: COMO DEUS É BOM! (Jinsi gani Mungu alivyomwema!).

VIDEO YA SR. SERAFINA

TV inayoitwa LIBERAL, inayounganishwa na mtandao muhimu wa Brazil yote, mwezi Oktoba mwaka huu ilifanya mahojiana na masista wetu Zelia Valentim na Jandira Barbosa, wanaohusika na ya Divina Providencia. Huduma hiyo inaonyesha picha za kazi inayofanywa na masista hao wawili katika Kituo cha Refugio San Gaspare kwa ajili ya wanawake wajawazito na wagonjwa. Madhabahu madogo ya Kanisa la Parokia la Altamira, Pará, ambalo limewkwa wakfu kwa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili, chini yake, yapo mabaki ya Sr. Serafina. Kwa kukamilisha wa kazi, TV ilimhoji Sr. Marilia, huko Belem, ikionyesha sehemu ya makumbusho ya Sr. Serafina, yaliyoko katika jumuiya ya Mama yetu wa Guadalupe, Belem. Video inayoonyesha ya shughuli za Sr. Serafina huko Altamira, na maendeleo ya mchakato wake wa kutangazwa mtakatifu inachukua muda wa dakika saba: ilionyeshwa huko Altamira na Belem, ilikuwa na mvuto kubwa. Katika video hiyo, Padre Ivan Conceição da Silva, mwanasheria za kanisa wa Belem, alizungumza juu ya umuhimu wa kutangazwa Mtakatifu kwa Sr. Serafina kwa Kanisa katika Amazonia.

Sr Marília Menezes, asc

Barua ya Dorothy Day yagudnduliwa kwenye Makumbusho ya Ruma



Watafiti na na watunza kumbukumbu mara nyingi huwa na ndoto na kufikiria kupata nyaraka hadi pale panapokuwa na uwezekano wa kuzipata, barua au magazeti yaliyofichika kwenye shelfu zilizosahaulika kwenye makumbusho.

Hivyo hata mimi nilshakuwa na ndoto ya kugudnua siku moja kitu kama hicho, nilifikiri isingenitokea hivyo kamwe, lakini mwishoni, siku ya tarehe 16 Novemba, niliona kwenye shelfu ya Sr. Angelita Myerscough (mimi ninafanya kazi kwenye makumbusho ya Ruma siku moja katika juma). Pale kwenye shelfu moja iliyosahaulika, kulikuwa na nyaraka sinazohusiana na Dorothy day na Harakati za Wafanyakazi Wakatoliki. Kati ya nyaraka hizo ipo barua ya mwaka 1938, iliyoandikwa kwa mkono na Dorothy Day kwa Sr. Angelita, kwa uangalifu ilihifadhiwa kwenye karatasi ya plastiki. Angelita alijua ni nini alichokuwa nacho mkononi, hata kama kwenye mwaka huo, alikuwa kijana mwabuduo mwenye nadhiri za muda mwaka mmoja.

Kwa kuwa nyaraka za Dorothy Day zimetunzwa kwenye makumbusho ya Chuo kikuu cha Marquette huko Milwaukee, niliwasiliana na Phill Runkel, Mtunza makumbusho anayetunza nyaraka zake, na huko nilituma nakala moja ya barua na bahasha. Phill aliniambia kuwa wanakusanya na kuandaa nyaraka za kutuma Roma kwa ajili ya mchakato wa kutangazwa mtakatifu Dorothy Day, kwa kuwa hakupata kamwe nyaraka zingine zinazofanana na zile za Dorothy Day na Sr. Angelita, siwezi kusema kuwa hii barua inaweza kujumuishwa na nyaraka zitakazotumwa Roma. Hadi hapa barua hii inaniacha na maswali mengi. Harakati ya wafanyakazi wakatoliki toka kwenye gazeti inaonekaka iliundwa tarehe 1 Mei 1933. Sr. Angelita hivyo alikuwa katika mawasiliano na DorothY Day tangu mwanzo wa uwepo wa harakati.

Sr. Angelita aliwezaje kufahamu harakati hiyo? Kitu gani kilikuwa “kwenye mkutano wa Mei” ambacho kinaongelewa kwenye Barua? Toka wapi Sr. Angelita alikusanya pesa za kutuma kwa Dorothy Day, kwenye

harakati ambapo kwa wakati huo alikuwa sista mwenye nadhiri za mwanzo? Ni akinani "arobaini" ambao wangetumiwa nakala za sala zilizotolewa na "Ade Bethune?" Sala ambayo inaongelewa imefichika kwenye sehemu nyingine ya makumbusho? Kwa hakika haipatikani kwenye shelfu ya Dorothy Day tuliyonayo. Ni akinanani wengine masita wa nadhiri za muda "arobaini"? Huu waraka, hata kama hauna maana sana ya kihistoria kwa ajili ya Harakati ya Wafanyakazi Wakatoliki ya Dorothy Day, lakini inaonesha kuwa Sr. Angelita alijali huduma kwa masikini na maana ya kina ya shukrani ya Dorothy Day kwa mmoja ambaye hakumufahamu binafsi. Mwandiko katika miaka hiyo ambapo ujumbe wa shukrani uliandikwa kwa mkono ilikuwa ni ishara ya heshima, barua hii inakazia jambo ni kwa namna gani hawa wanawake wawili ni mifano mahususi kwa wengi wetu. Kwa kufanya utafiti zaidi kwenye makumbusho kwaweza kutusaidia kupata majibu au nyaraka zingine zinazofanana na hizo. Hadi hapo kile ambacho ni muhimu ni kwamba barua ilishapatikana na ni ya kwetu.

Sr Regina Siegfried, asc

Barua ya Dorothy Day kwa sista Angelita

Mai, 15

Mpendwa Sr. Angelita,
Hapa ofisi imetunza barua yako nzuri hadi kurudi kwangu toka katika safari ya kikazi, ambapo nimechelewa natumaini utanisamehe. Ningeweza lakini kukujulisha.
Mimi siwezi kujieleza ni kwa jinsi gani barua yako ilivyotugusa, zaidi ya yote kujali kwako na tunatoa shukrani zetu nyingi kwa sala zako. Sala zenu ni kama nguvu za kituo cha umeme. (Unajua inatosha kazi ya watu 30 kwenye kituo cha umeme kumulika Manhattan yote?) wakati mwingine ninasikia nguvu ya toleo la sala na la sadaka za marafiki kama wewe.
Tafadhali endelea kusali kwa ajili yetu sote, kwa ajili ya nyumba zetu za wageni, kwa ajili ya vilema, kwa ajili ya wale wote waliokwama, kwa ajili ya vipofu walioko kati yetu (tukiwemo hata sisi).
Nafikiri kuwa barua hii itafika kwa kuchelewa kwa ajili ya kile ambapo kingepaswa kuwa "mkutano wako wa Mei" na nasikitika. Ni kwa sababu kila mmoja alifikiri labda ni muhimu zaidi mimi binafsi kujibu ambapo hakuna aliyefanya hivyo.
Hapa zipo sala mbili ninazopendelea, nilizopewa na Abe Bethune mwenyewe. Labda unaweza kuwapa wengine arobaini ambao wamekuwa wema hivyo, ili waweze kutoa nakala.
Toa shukrani zangu kwa wote kwa msaada wenu, na kwa pesa ambazo mlinitumia. "Upendo ni badilishano la zawadi". Na kama anavyosema Mt. Ignazio, endeleeni kuombeana.

Katika Kristo,
Doroty Day



Eneo la Bara: Amerika
Region: USA

Hongera kwa siku ya kuzaliwa

J
umatano ya 8 Novemba, Sr. Leonia Riebel aliadhimisha miaka mia ya maisha, rafiki yake Monsignor Walter Rossi, wa Washington DC, aliongoza adhimisho la Misa Takatifu kwa ajili yake, kwenye kanisa la "Agano Jipya" huko Wichita.
Hongera Sista Leonia kwa tukio hili la furaha.
Katika picha, kutoka kushoto ni Monsignor Walter Rossi, ambaye alifanya kazi naye kwenye Santuari ya taifa, dada yake Florentia, asc, mwenye umri wa miaka 101, Sr. Jan Renz na Sr. Diana Rawlings na dada mwingine Sr. Barbara, asc, mwenye umri wa miaka 93.

Sr Nylas Moser, asc
Sr Fran Schumer, asc

Eneo la Bara: Ulaya
Region: Wroclaw

...Kwa Neno lako... Tunapokea changamoto za Hati ya Mkutano Mkuu wa XXI, 2017.

Hii ilikuwa ni mada ya Mikutano ya majiundo kwa ajili ya masista ASC wa Region yetu ambayo ilifanyika katika makundi mawili kuanzia 6 hadi 8, na kuanzia 16 hadi 12 Novemba 2017 kwenye nyumba ya Boleslawiec. Mikutano iliongozwa na masista walioshiriki Mkutano Mkuu.

Mkutano wa kundi la kwanza uliongozwa na sr. Ewa Cleps Mkubwa wa Region, Sr. Elzbieta Kumatowaska – Mshauri wa Region na Sr. Teresa Jaszczyszyn, mjumbe, na mkutano wa kundi la pili uliongozwa na Sr. Ewa Claps na Sr. Elzbieta Kumatowaska.

Masista hawa waliokuwa wajumbe wa mkutano mkuu walitushirikisha mang'amuzi yao yenye utajiri ya muda mrefu wa mkutano mkuu. Walitushirikisha kazi walizozifanya katika siku za mkutano na tulielewa umuhimu wa maandalizi, wa uchambuzi, wa mazungumzo, wa umakini na bidii ili kupata Hati ambayo tumekabidhiwa ambayo yaweza kuwa sauti ya Shirika zima.

Sr. Ewa akisoma barua ya ubainisho na kuwasilisha hati ya Mkutano Mkuu, aliweka mkazo katika maneno muhimu kwa ajili ya

kufanyia kazi Hati. Kuishi katika hali ya malezi endelevu, kuwa makini na "Nguvu ya kinabii ya NAMNA GANI", kujenga mahusiano ya kiinjili.

Baada ya sherehe ya makabidhiano ya Hati, yaliyotanguliwa na wimbo "Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga katika njia yangu" na somo kutoka katika sehemu ya Injili ya Luka (5: 1-11) ulitolewa muda kwa ajili ya kusoma upya hati ya Shirika letu. Siku iliyofuata, tukitumia yale yaliyomo kwenye Hati, tulifanya kazi katika makundi manne, tukijibu maswali yafuatayo:
1. Ni mambo gani Hati ya Mkuutano Mkuu inaniita kwa ajili ya kuanza mchakato wa mabadiliko?
2. Ni kwa namna gani jumuiya ASC inaweza kujibu hizi changamoto?
3. Ninapokeaje Hati ya Mkutano Mkuu wa XXI?

Majumuisho ya majibu yatatumika wakati kikao cha Mkutano wa Region ambao utafanyika kuanzia 12 hadi 14 Januari 2018.

Wakati wa mikutano tulishiriki Misa iliyoadhimishwa na Padre Adam Langkamer – pljar. Kila mshiriki alipata muda kwa ajili ya sala binafsi, kuabudu pamoja Sakramenti Kuu na sala za masifu.

Mwishoni mwa mikutano ya malezi, wakati wa Misa, tulisali kwa ajili ya masista walioadhimisha miaka 60 ya nadhiri zao za kitawa, Sr. Malgorzata Braszko, Sr. Magdalena Karaban, Sr. Lucja Partyka na Sr. Marianna Konefal. Tulisali pia kwa ajili ya masista wa kundi hili ambao walishafariki, Sr. Roza Abramek na Sr. Esther Chlastawa, tukiomba kwa ajili yao huruma ya Mungu na ukamilifu wa maisha pamoja naye katika furaha ya mbinguni.

Nafikiri kuwa masista walirudi katika jumuiya zao kwa tafakari juu ya upekee wa maisha katika jumuiya ya kitawa, yaliyojengwa juu ya tasaufi ya Damu ya Kristo na juu ya uaminifu kwa karama ya Maria De Mattias.

Maombi ya Mama Mwanzilishi wetu na Baraka za Mungu zifungue nyoyo zetu, ziangaze njia na kutupa ujasiri kwa ajili ya kutekeleza utume kama Waabuduo Damu ya Kristo.

Katika umoja wa kuabudu Damu ya Kristo,

Sr Bernadetta Pajdzik, asc

Na Bwana anataka nini kwako...
Kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako! (Mika 6:8)

Kama yule anayehusika kwa sasa na Haki, Amani na Mshikamano wa Viumbe (Giustizia, Pace e Integrità del Creato (GPIC)) kwa upande wa Uongozi Mkuu, hivi karibuni nilipata nafsi ya kushiriki kwenye Semina ya mwaka ya malezi kwa ajili ya wahamasishaji wa GPIC, iliyofathiliwa na Tume ya Umoja wa Kimataifa wa Mama Wakuu.

Semina ilifanyikia Roma, ikiwa na washiriki kutoka nchi mbalimbali 20. Baadhi ya washiriki, kama mimi ni wakazi wa Roma na ni wale walio katika uongozi mkuu wa mashirika mbalimbali, lakini wengine wengi walikuja kutonga pembe mbalimbali za dunia na wanafanya utume wa kuwa wajumbe wa GPIC kwa ajili ya jumuiya zao. Semina ilipangwa kwa ajili ya kutoa habari, kuendeleza ujuzi, kupanga na kuhamasisha kazi katika mtandao kati ya wale ambao wanahusika katika kazi ya ushirikiano wa kimataifa kwa ngazi ya GPIC. Napaswa kusema kuwa katika kipindi cha siku tatu ambapo tulikuwa pamoja, tulifanya hayo… na mengine mengi.

Kati ya mambo mengi yaliyojadiliwa kulikuwa na; GPIC kama maendeleo muhimu ya kibinadamu, Laudate Sì naTafakari, GPIC katika nadhiri za kitawa na katika maisha ya kitawa ya kinabii, Wajibu, muundo na mtandao wa GPIC, Tazama, Hukumu, tenda kama kiongozi kwa ajili ya mpango wa kichumgaji na mashirikisho ya shughuli bora za GPIC. Zaidi ya hayo, tulipanua ufahamu na uelewa wetu wa GPIC kupitia sala za mashirikisho, majadiliano katika makundi madogo na kichekesho cha kiutamaduni saa za jioni.

Semina yote ilikuwa mwito endelevu wa kuishi roho inayounganisha ya GPIC, yaani kutofanya kitendo na shughuli kwa kujitenga, bali ku-

sikia Haki, Amani na Mu-unganiko wa Viumbe kama sehemu muhimu ya fikra zetu, mwendo wa moyo. Kwa upande wetu Waabuduo ni kukuza karama yetu "kwa kuwa uwepo wenye huruma, unaopatanisha… kwa moyo makini kwa kilio cha Damu". (Hati 2017).

Kama tunasikiliza Neno la Mungu kwa kina, tutasikia kuwa tunapaswa siyo tu kuhamasisha haki bali tunapaswa kuishi kwa haki, kwamba hatupaswi tu kuongea juu ya amani bali matendo yetu yanapaswa kuwa ya amani na siyo ya uonevu, kwamba hatupaswi tu kusali sala ya shukrani kwa ajili ya zawadi ya viumbe, bali matendo yetu ya kila siku yanapaswa kuonesha utunzaji wetu wa nyumba yetu ya pamoja ambamo tunaishi. Tunaweza kuongea na kuelezea Injili, bali tusipoishi mfano halisi wa Kristo katika uhusiano wake na masikini, kama mwokozi, kama yule anayetoa changamoto kwa miundo ambayo haisaidii kuleta heshima ya kibinadamu, maisha yetu hayatakuwa ya kinabii.

•Kitu gani ni muhimu sasa kwetu sisi Waabuduo Damu ya Kristo kwa kuishi kweli tasaufi yenye haki, amani na utunzaji wa viumbe kama jibu kwa mwito wa Damu?

•Katika kutafakari juu ya Hati yetu ya 2017, TUKOJE "tukiishi katika ushirika na masikini, waliotengwa na wale wanaoishi pembezoni mwa jamii "na zipi ni chaguzi tunazopaswa kufanya ili" kuongeza shughuli zetu kwa ajili ya haki, amani na mashikamano wa viumbe?

•Na nakuomba utufahamishe… Tunawezaje, kama Uongozi Mkuu, kusaidia, kuahamasisha na kubaki nawe, dada zetu kwenye Region na Foundation, wakati tunapobadili ulimwengu katika roho ya Injili katika utume na kazi za kitume tukitenda haki, amani na utunzaji wa viumbe?

Kama unataka habari zaidi juu ya mojawapo ya hoja hizi zilizowasilishwa kwenye semina, tunakuomba utufahamishe na utafurahia kushirikishwa utajiri na yale yote ambayo niliyapokea… tunajifunza kutoka kwa wengine wakati tunapofanya kazi pamoja "kuelekea ule mpango mzuri wa vitu".

Sr Dani Brought, asc

Kalenda

ya Uongozi Mkuu

4 Disemba,Sr. Matija Pavić, Sr. Dani Brought, Sr. Bridget Pulikakunnel watamsindikiza Sr. Patrizia Pasquini kwenye jumuiya mpya huko Castelplanio.

9 Disemba: watashiriki kwenye ritiriti ya Majilio ya Jumuiya ya kimataifa.

11 Disemba: Sr. Nadia Coppa na Sr. Wieslawa Przbyło watarudi Roma baasa ya ziara huko Tanzania.

13 – 15 Disemba: mkutano wa malezi ya mwingiliano wa tamaduni wa uongozi mkuu utakaoongozwa na Sr. Marian Marcia Pineiro, HFB.

17 Disemba: ushiriki kwenye tamasha la nyimbo za Krismasi kwenye Kanisa la Damu Azizi.

27 Disemba – 20 Januari: Sr. Dani Brought atafanya ziara kwenye Foundation ya Bolivia na atakuwa na mapumziko huko USA.

6 – 17 Januari: Sr. Bridget Pulikakunnel na Sr. Wieslawa Przbyło watafanya ziara kwenye Region ya Wroclaw.

11 -12 Januari: Sr. Nadia Coppa atashiriki mkutano wa mwaka wa umoja wa Mama wakuu- Roma.

15 – 31 Januari: Sr. Nadia Coppa na Sr. Matija Pavić watatembelea Region ya Italia.

Waliorudi nyumbani kwa Baba

Region ya Italia
16 Disemba 2017
Sr Bruna Ziotti

Region ya Italia
18 Disemba 2017
Sr Maddalena Orlando

Region ya USA
22 Disemba 2017
Sr Helen Ridder

Pongezi kwa uongozi mpya wa Foundation ya Korea

Utakaoanza kazi Januari 2018 – 2023

Sr. Hee Kyung Julianna Kim – Coordinator
Sr. Mi Sook Francesca Kwak – Mshauri
Sr. Kyung Mi Rosa Kim – Mshauri

Mikutano ya Region

12- 14 Januari 2018: Mkutano wa XV wa Region ya Poland
26 – 29 Januari 2018: Mkutano wa V wa Region ya India

Mikutano ya Foundation

4 – 7 Januari 2018: Bolivia
10 – 12 Januari 2018: Argentina

Tangu mwanzo wa wito wangu nilijisikia kuiba moyo wa mpendwa Msulubiwa, na kuanzia hapo na kuendelea, nimejaribu daima kufa kishahidi kwa wivu, na sitafurahi kamwe kama moyo wangu wote hautakuwa wa Yesu.

MDM, 26 Novemba 1850